**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 24 Mei, 2021.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa Mwaka 2021/2022.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kuhusu Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa Mwaka 2021/2022.

## II. **MASWALI:**

**Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera na Uratibu wa Baraza la Wawakilishi.**

65. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera na Uratibu wa Baraza la Wawakilishi:

Katika Shehia ya Bumbwisudi eneo la Goa hadi uwanja wa mpira, kila zinaponyesha mvua kubwa wananchi wa maeneo hayo huwa wanakabiliwa na mafuriko makubwa. Hali hiyo husababisha kero na hasara kubwa, na imewahi kuripotiwa mara nyingi kwa viongozi mbali mbali wa Wizara, hata hivyo tatizo hilo bado linaendelea.

Kwa kuwa tatizo hili ni la muda mrefu Je, Serikali inawaahidi nini wananchi wa Shehia ya Bumbwisudi.

**Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:**

90. MHESHIMIWA MOHAMED MGAZA JECHA (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Kwa kipindi kirefu, Serikali ilikodi nyumba katika eneo la Mkoani Mbuyuni kisiwani Pemba kwa ajili ya kutoa huduma ya kurekebisha tabia za wananchi walioathirika na utumiaji wa madawa ya kulevya (Sobber house). Lakini kwa bahati mbaya, nyumba hiyo kwa sasa haitumiki tena kwa utoaji wa huduma hiyo.

(a) Je, ni sababu gani zilizopelekea nyumba hiyo kutoendelea na utoaji wa huduma.

(b) Je, kwa nini Serikali isitafute njia mbadala ya kujenga nyumba yake ili kuepusha gharama za kodi za kila mwaka.

(c) Je, Serikali inazo nyumba ngapi Unguja na Pemba zinazoendelea kutoa huduma hiyo.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

107. MHESHIMIWA MTUMWA PEYA YUSSUF (Jimbo la Bumbwini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kituo cha afya Kiongwe kina changamoto ya uhaba wa daktari ambapo kituo hicho kinaonekana kinatoa huduma kwa wagonjwa wengi katika eneo hilo tofauti na huko nyuma tulikotokea, ukiangalia hivi sasa kuna daktari mmoja tu anaetoa huduma.

(a) Je, Wizara inalijua hili.

(b) Je, Wizara inawaahidi nini wananchi wa eneo hilo.

(c) Je, ni lini ataletwa daktari mwengine ili kusaidiana na daktari aliyepo.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

211. MHESHIMIWA RUKIA OMAR RAMADHAN (Jimbo la Amani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi Rais, Fedha na Mipango:

Tume ya Pamoja ya Fedha imeundwa kwa mujibu wa Ibara ya 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na pia kupitia Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha, sura ya 140 ya mwaka 1996.

(a) Je, kuna mapendekezo na ushauri gani ambao upo kisheria kuhusu uhusiano wa kifedha baina ya pande mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ)

(b) Je, kuna asilimia ngapi ya mapato ambayo SMZ kupitia Wizara ya Fedha na Mipango inayapata na kwa muda gani asilimia hiyo kukamilika.

(c) Kwa mazingira ya sasa na maendeleo tunayoyahitaji, Je, hatuoni ipo haja ya kupitia upya mfumo huo wa Kisheria wa kuchangia na kugawa mapato baina ya SMZ na SMT kupitia Wizara za Muungano.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

196. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali

Kumekuwa na upungufu mkubwa wa walimu wa skuli za msingi katika Jimbo la Nungwi.

(a) Je, kuna vigezo gani vinavyotumika kuwagawa walimu wa skuli za msingi katika Jimbo la Nungwi.

(b) Je, ni utaratibu gani wanaoutumia Maafisa katika kutekeleza jukumu la kugawa walimu hao.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

191. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani)-

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Barabara ya Ukutini hadi Mtangani bandarini ni barabara iliyowahi kupata ufadhili wa kuwekwa kifusi na MIVARF. Hata hivyo, kwa muda mrefu sasa barabara hiyo haiko vizuri na hali yake ni mbaya.

(a) Je, ni lini barabara hiyo itajengwa kwa lami.

(b) Je, ni lini utaitembelea ili kuona uhalisia wake.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

175. MHESHIMIWA HAROUS SAID SULEIMAN (Jimbo la Wete) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Miongoni mwa changamoto za Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) kwa upande wa Pemba ni kukosekana kwa Afisa Masoko (Marketing Officer) ambaye pamoja na mambo mengine angefanya kazi ya kulitangaza Shirika kutanua soko pamoja na kuongeza mapato ya Shirika hilo kupitia bidhaa zinazozalishwa.

(a) Je, ni hatua gani zilizofikiwa katika kuhakikisha Afisa Masoko wa Shirika la ZSTC, Tawi la Pemba anaajiriwa.

(b) Je, Shirika linajitangaza vipi pamoja na bidhaa zinazozalishwa katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

36. MHESHIMIWA SHAMATA SHAAME KHAMIS (Jimbo la Micheweni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatekeleza kwa vitendo Ilani ya CCM pamoja na mikakati yake mbali mbali katika kuuinua uchumi wa Zanzibar hasa kupitia Uchumi wa Buluu.

(a) Je, Wizara hii ina wafanyakazi wangapi katika Wilaya ya Micheweni.

(b) Je, wavuvi wanapohitaji taaluma inayohusiana na Uchumi wa Buluu, waende Ofisi gani katika Wilaya ya Micheweni.

(c) Je, Wizara inatoa mchango gani kusaidia wavuvi wanaopata kadhia ya kupoteza maisha au kupotea baharini.

**Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:**

153. MHESHIMIWA SULUBU KIDONGO AMOUR (Jimbo la Mkwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Wananchi wa Jimbo la Mkwajuni wenye taaluma ya Afya wamekuwa wakijitolea kwa miaka mingi sasa katika kutoa huduma ya afya bila ya kuajiriwa katika vituo ndani ya jimbo hilo.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia ajira wataalamu hao wa afya waliojitolea kwa muda mkubwa sasa.

(b) Je, vigezo gani vimetumiwa na Serikali kuhakikisha wataalamu wote wa afya wanaojitolea wanapata fursa sawa sawa wakati wakutolewa ajira hizo.

**III. <u>HOJA ZA SERIKALI:</u>**

**<u>Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:</u>**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka 2021/2022.

**Zanzibar,**
**24 Mei, 2021.**

**(Raya Issa Msellem)**
**<u>KATIBU WA BARAZA</u>**